# NADHARIA YA MAISHA YA MTI NA MTU

ISBN 978-9976-5-7130-1

Mwanawetu Mmuni

# DECLARATION AND COPYRIGHT

I, MWANAWETU MMUNI, declare that; this theory is my own original work and it has not been presented anywhere or will not be presented to any other institution for any award.

Signature: M. A. Mmuni.

Date: 2nd June 2016

This theory should not be reproduced by any means, in full or in part, except for a short extract in fair dealings for research or private study. Critical scholarly review or discourse with an acknowledgement. Without written permission of **MWANAWETU MMUNI**

# YALIYOMO


DECLARATION AND COPYRIGHT ..... 2
UTANGULIZI ..... 4
WASIFU ..... 5
SEHEMU YA KWANZA ..... 7
1.0 KIUMBE HAI CHA KWANZA KUITAWALA DUNIA ..... 7
1. 1 ELIMU YA KUTAWALA DUNIA ..... 8
1. 2 HEWA/ KUPUMUA ..... 9
1. 3 KUBADILISHA NGUVU ZA JUA KUWA NGUVU ZA MWILI ..... 10
MASWALI ..... 11
SEHEMU YA PILI ..... 14
2.1 MAKAZI (NADHARIA YA MAKAZI) ..... 15
2.1.1 MUONEKANO NA UWEZO ..... 16
2.1.2 ULINZI NA USALAMA ..... 17
2.1.3 MAZINGIRA ..... 19
2. 2.0 NADHARIA YA MAISHA “UHAI” ..... 20
KUZALIWA HADI KUFA ..... 20
2.2.1 MBEGU ..... 20
2.2.2 UKUAJI ..... 21
2. 2.3 UVUMILIVU ..... 22
2.3 ASILI/ KURITHI ..... 23
2.4 MAJANGA NA ASILI ..... 25
(NADHARIA YA MABADILIKO YA MWENENDO WA MAISHA) ..... 25
2.5 MATUNZO/ULINZI ..... 26
MATUNDA BORA ..... 28
2. 6 TABIA KATI YA MITI NA MTU ..... 29
JENDWALI 1.1 MFANANO WA ASILI YA MITI NA MTU ..... 30

# UTANGULIZI

Nadharia hii ya MAISHA YA MTI NA MTU pamoja na ushahidi wake; inamtambulisha kiumbe cha kwanza kuitawala dunia ambacho ni mti. Kabla ya mtu kuishi duniani ulianza kuishi mti. Pia inaeleza mlingano wa mti na mtu kuwa ni viumbe vyenye asili moja na kutofautiana muonekano na maumbile. Viumbe hai hivi viwili (mti na mtu) vinashirikiana lakini havitegemeani isipokuwa mtu anautegemea mti kupata uhai. Bila mti hakuna uhai wa mtu.

# WASIFU

Bi. Mwanawetu Mmuni, nimezaliwa tarehe 05/02/1983 mkoani Lindi. Kwasasa ninaishi Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani mkoani Mtwara.

Kazi yangu tofauti na utunzi na uandishi wa vitabu, ni Ualimu. Nimeajiriwa na Serikali kuwa Mwalimu wa sekondari baada ya kuhitimu shahada yangu ya kwanza ya Elimu yaani *Bachelor of Arts with Education* (B.A.ED) mwaka 2010 katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam (MUCE) mkoani Iringa.

Shule nyingine nilizosoma ni Dakawa High School kidato cha sita mwaka 2004 mkoani Morogoro, Shule ya Sekondari Utete (UMAKURU) kidato cha nne mwaka 2001 mkoani Pwani, na Shule ya Msingi Mingoyo na kuhitimu Elimu ya Msingi mwaka1996 mkoani Lindi.

**NADHARIA HII INA SEHEMU KUU MBILI NAZO NI;**

1. KIUMBE HAI CHA KWANZA KUITAWALA DUNIA

2. MLINGANO WA MAISHA YA MTI NA MTU

# SEHEMU YA KWANZA

## KIUMBE HAI CHA KWANZA KUITAWALA DUNIA

### 1.0 KIUMBE HAI CHA KWANZA KUITAWALA DUNIA

Kiumbe hai cha kwanza kuitawala dunia ni mti. Kabla ya binadamu kuishi na kuitawala dunia, ilianza kuishi miti ndipo watu na viumbe hai wengine walipoweza kuishi.

Ushahidi wa maisha ya Mti na Mtu kuwa na asili moja, na miti ndiyo viumbe wa kwanza kuitawala dunia ni kama ifuatavyo;-

## USHAHIDI WA MTI KUWA KIUMBE CHA KWANZA KUITAWALA DUNIA

### 1. 1 ELIMU YA KUTAWALA DUNIA

Binadamu alitegemea miti katika kila kitu ndipo alipoweza kuishi na kujifunza namna gani miti imeweza kuitawala dunia. Kama angelianza kuishi mtu, mti usingeliweza kuiga na kuishi maisha yanayofanana na ya mtu kwa kuwa mti hauna uwezo wa kujifunza bali inategemea uwezo wake wa asili.

Hivyo endapo miti yote itaangamizwa na kubakia binadamu na viumbe vingine pekee, hakutakuwa na maisha kwa viumbe hai lakini watu wakitoweka duniani, miti itaendelea kuishi na kuitawala dunia na viumbe vingine.

## 1. 2 HEWA/ KUPUMUA

Hewa ya oxygen ambayo inatumiwa na binadamu kupumulia, inapatikana duniani baada ya kuzalishwa na miti (mimea) pekee. Hivyo (miti) mimea ikitoweka, viumbe vyote vinavyotegemea gesi hiyo ili viweze kuishi, vitaangamia.

Wanasayansi wanahusianisha maisha ya binadamu na miti kwa kubadilishana hewa kwa njia ya upumuaji. Hivyo bila miti / mimea, hakuna maisha kwa binadamu. (Binadamu kupumua /kutoa) gesi ya Carbondioxide na kuvuta oxygen wakati miti inavuta Carbondioxide ambayo itaisafisha na kuirudisha tena duniani ikiwa safi (Oxygen).

Hivyo basi, mti/mmea ni kiwanda cha kusafishia hewa / gesi inayotumika na viumbe hai vingine ili viweze kupata uhai. Miti haitegemei kuishi na kuendelea kupata uhai kwa kuvuta (kupumua) hewa / gesi ya Carbondioxide kutoka kwa mtu au viumbe vingine hai vinavyovuta gesi ya Oxygen na kutoa/ kupumua gesi ya Carbondioxide bali mti unaweza kupata gesi hiyo kutoka kwenye vyanzo vingine.

### 1. 3 KUBADILISHA NGUVU ZA JUA KUWA NGUVU ZA MWILI

Kiumbe pekee duniani chenye uwezo wa kisayansi wa kubadilisha nguvu za jua kuwa nguvu inayohitajika katika miili ya viumbe hai wengine ni miti / mimea.

Kama Wanasayansi wanavyoeleza kuhusu sayansi ya lishe kuwa; mnyororo wa thamani ya nguvu za mwili kutoka kwenye jua kwenda kwa viumbe hai vyote duniani, unaanza kwa mimea halafu viumbe hai vingine vinapata nguvu hiyo kwa kula mimea au kula kiumbe kilichokula mimea.

## MASWALI

A. Kwanini ukienda kuomba (kutambika mizimu) kwenye miti mikubwa unapata nafuu au kupona maradhi au kutoweka kwa shida mbalimbali?

B. Kwanini binadamu anapoangalia majani ya mti kwa muda mrefu ni tiba?

**Majibu**

**Kisayansi**; Kuangalia majani kwa umakini (concentration) kwa muda mrefu ni tiba kwa kuwa kunatuliza fikra (akili) na mwili hivyo matendo yote ya mwili ya hiyari yanasimamishwa na kuruhusu hewa safi (Oxygen) kuingia mwilini.

**Utamaduni; Kijadi matambiko hufanywa kwenye miti mikubwa wakiamini huko ndiko iliko mizimu ya watu wao wa kale.** Ukweli hakuna mtu yeyote wa kale katika mti wowote zaidi ya wao wenyewe (new generation) watakaokwenda kuishi mtini pamoja na vitu vyao vyenye nguvu kadri ya nguvu za mtu aliyeviweka.

**Kwa njia hii ya utamaduni wanafanikiwa kwasababu kuna haya yafuatayo**;

**IMANI**: Uwezo mkubwa wa nguvu za asili za mti katika kulinda na kutunza dunia ndicho ambacho mtu hawezi kuwa nacho sababu nae ni miongoni mwa mazingira yanayotunzwa na miti/mimea. Vitabu vya dini vinaeleza……… "Mti wa uzima" hakuna historia ya mtu kutoa uzima kwa binadamu mwenzake. Hivyo imani za dini mbalimbali zimewaaminisha waumini wao ya kuwa, kuna nguvu na uwezo wa miti katika uponyaji na uharibifu kwa binadamu.

***Ushahidi;*** Mtu aliyelelewa na kutunzwa katika miongozo ya imani / miiko kama vile dini, uchawi, jadi na desturi mbalimbali katika jamii. Endapo mtu ataamini na kujiimarisha katika mwongozo wa imani hiyo au hizo naye atakuzwa na kujengwa katika misingi hiyo na itamletea mafanikio. Kinyume chake iwapo atakiuka miongozo iliyomjenga, atapata madhara makubwa. Tofauti na mtu ambaye hakulelewa wala kujengwa katika imani fulani, akaenda kinyume na imani hiyo kuna uwezekano mkubwa wakutopata madhara yoyote.

**NGUVU YA FIKRA YA UTEGEMEZI**: Nguvu kubwa iliyopo kwenye fikra za Mtu kwa kile anachokitegemea kupata mahitaji muhimu. Saikolojia ya binadamu katika kutegemea uwezo na rika.

**USHAHIDI**

UWEZO; Maskini wote katika dunia wanawategemea matajiri ingawa wanajikimu wenyewe kwa jasho lao na haitatokea tajiri akamtegemea maskini ingawa utajiri hauwezi kuwepo bila jasho la maskini.

Utajiri hujenga kiburi. Tajiri anaweza kuacha kuwatumikisha maskini akabuni mashine badala yao hivyo kujenga woga kwa maskini na kujikuta wakiendelea kunyenyekea.

Hivyo Mtu anategemea mti kupata mahitaji kama vile; chakula, dawa, samani za nyumbani na ofisini, kivuli, hewa safi (Oxygen), kutunza vyanzo vya maji na makazi ya viumbe wengine. Hali ya mti kutegemewa na mtu ni kubwa kuliko mti unavyomtegemea mtu. Ingawa kuna miti michache inaweza kukuzwa kwa kutegemea msaada wa binadamu kama ilivyo kwa kiwanda kuhitaji wafanyakazi wakuendesha mitambo. Hivyo mtu hunyenyekea mti kutokana na uwezo wake.

**RIKA NA UNASABA**

*Rika*; Inathibitisha uwepo wa mtu au kitu na umuhimu wake katika maisha. Matambiko au ibada zinafanyika / yanafanyika kwenye miti iliyopea sio michanga. Pia katika kila jamii inayosujudia matambiko lazima iwe na kiongozi, mara nyingi anatokana na wazee walioishi eneo ambalo mti umeishi na sio mgeni. Sababu;

*Unasaba*: Mti unakuwa na nguvu kwa kiumbe kinachokisaidia kukipa uhai kwa asilimia kubwa. Mzee na mti mkongwe umekua pamoja au mtu ameukuta mti huo. Mti ulimpa pumzi binadamu huyo kuanzia mwanzo wa maisha yake yaani kutungwa kwa mimba yake, kukua kwake hadi anafikia umri wa ukongwe. Hivyo basi; damu ya binadamu huyo mkongwe ina kiwango kikubwa cha Oxygen kilichozalishwa na mti huo kwa maana rahisi wanakuwa naunasaba kama ambavyo anakuwa nao mama na mtoto.

***Ushahidi***; Kiumbe kilichochangia uwepo wa kiumbe kingine kwa kiwango kikubwa kinauwezo wa kukijenga au kukiharibu kiumbe kipya bila ya uhusiano wa shughuli za kisayansi. Kama vile laana ya wazazi hasa mama kwa watoto wao ambayo inatolewa kwa maneno na sio vitendo na kusababisha kiumbe kipya (mtoto) kulaanika. Pia hisia za mzazi pindi mtoto wake anapopatwa tatizo ingali bado hajapewa taarifa juu ya shida iliyotokea (Intuition feelings).

# SEHEMU YA PILI

# MLINGANO WA MAISHA YA MTI NA MTU

## 2.1 MAKAZI (NADHARIA YA MAKAZI)

Makazi ya miti ni *misitu*, *mapori*, na *vichaka*; yaweza kuwa ya asili au ya kupandwa na binadamu. Na makazi ya binadamu ni '*high density',* na *'low density'* kwa makazi yaliyoandaliwa na mipango miji, pia kuna 'squatters' na vijiji.

**USHAHIDI WA MAKAZI YA MTU (MIPANGO MIJI) KUTOKANA NA MAKAZI YA MTI**

### 2.1.1 MUONEKANO NA UWEZO

Mpangilio wa miti iliyotengeneza **msitu** wa asili inajipanga katika mistari kulingana na uwezo wa Mti (uwezo wa mizizi, kupata mwanga na hewa) katika kutawala eneo la kutosha na kuwa na kimo na ujazo unaofanana mfano ni misitu yote ya asili duniani kote. Mara nyingi miti ya aina moja ndiyo inayoweza kutawala eneo moja na aina nyingine hujitenga. Ni sawa na makazi ya binabamu '**low density'**. Nyumba zote zinajengwa kwa mpangilio na hutenganishwa na barabara za mitaa kila upande hivyo kuonekana zenye nafasi ya kutosha kutoka nyumba moja hadi nyingine. Mfano Tanzania; makazi haya yapo Masaki, Mikocheni, Samora katika jiji la Dar-es-salaam. Maeneo haya utawaliwa na watu wenye uwezo mkubwa wa kifenda (kipato) na matokeo yake kunakuwa na makazi/ nyumba zenye muonekano unaofanana.

**Mapori**: Yanamiti mchanganyiko yenye vimo na ujazo tofauti yaani mikubwa, midogo, myembamba pia inaambatana na (*uoto mwingine kama nyasi).* Ni sawa na makazi ya binadamu katika '**high density'**; ingawa eneo hili linakuwa limepimwa lakini watu wake huwa na uwezo wa kadri hivyo kukiuka sheria za majenzi na matokeo yake mtaa unakuwa na nyumba zenye muonekano tofauti. *Ghorofa* na nyumba za kawaida zinajengwa katika sehemu mmoja. Pia matumizi mengine ya ardhi tofauti na makazi yanafanyika katika maeneo haya *(magenge, bustani ndogondogo na biashara za kutembeza).* Mfano Ubongo, Kimara, Mbagala katika jiji la Dar-es-salaam.

**Vichaka**: Katika eneo hili miti na uoto mwingine hurundikana pamoja. Miti inayotengeneza vichaka huwa na miiba na mingine ni mitambaazi. Mara nyingi kuna kuwa hakuna nafasi yakupita kwenda upande wa pili wa kichaka hadi uzunguke eneo lote. Ni sawa na makazi yasiyopimwa (**squatters**), kuna kosekana hata njia/vichochoro vya kufika mtaa wa pili hadi uzunguke mtaa. Mfano Mazense katika jiji la Dar-es-salaam.

### 2.1.2 ULINZI NA USALAMA

**Misituni** kuna usalama mkubwa kwa kuwa wanyama wakali hawapendelei kuishi katika misitu kama ilivyo mbugani. Kwa sababu msituni sio eneo rafiki kwa wanyama (Herbivorous) kwa kuwa hakuna malisho (nyasi) hivyo wanyama wakali (Carnivorous) ambao wangefuata malisho kwa kuwinda wanyama hao nao hukosekana. Viumbe wakali katika eneo hili ni nyoka wakubwa kama chatu, anaconda, vifutu, na mamba kwenye mito na mabwawa. Wanaishi humo kwa sababu wanafuata ubaridi unaotokana na vivuli vya miti, unyevu na huwepo wa chakula (viumbe vidogo) kama digidigi na panya walioshindwa kuishi katika mapori na kutorokea msituni. Nyoka hawa sio wakali, hata ikitokea kwa bahati mbaya *ukamkanyaga* kuna uwezekano wakutokudhuru. Ni sawa na **ulinzi na usalama** uliopo katika makazi ya '**low density'** ni mkubwa sababu kuna nafasi kutoka nyumba moja hadi nyingine hivyo ni ngumu kwa mharifu kujificha. Pia walinzi wanaolinda maeneo haya ni wale wa ngazi ya juu kulingana na uwezo na thamani ya mali zilizowekezwa katika eneo hilo. Mara nyingi viongozi hawa wa ulinzi na usalama wanaweza kumsamehe *mvunja sheria kwa bahati mbaya* kisha kumuelimisha na kumuacha aondoke. Na kwakuwa wakazi waliowengi wa eneo hili ni viongozi, wafanyabiashara, na watu wengine wenye kipato cha juu; huweza kuajiri walinzi wa ziada kwa ajili ya nyumba zao, familia zao na wao wenyewe hivyo ulinzi na usalama ni mkubwa.

Kwenye **mapori** (Mbugani) usalama hakuna, muda wowote na popote ni hatari. Wanyama wakali wote yaani simba, chui, fisi, nyoka wakali, wadudu kama manyigu na nyuki wanaishi porini na vichakani. Viumbe vingine kama *ng'e, tandu, funza* hupenda kuishi kwenye magome ya miti iliyokauka. Hivyo viumbe wanaoishi au kupita kwenye maeneo hayo, wanahitaji tahadhari kubwa kulinda usalama wao. Ni sawa na **ulinzi na usalama** uliopo katika maeneo ya '**high density'**, usalama ni mdogo kwa kuwa makazi haya yanaruhusu kuishi watu wenye uwezo (vipato) tofauti hivyo wengine huingiwa na tamaa na kuanza kutishia usalama wa wenzao. Hivyo wakazi wengine wanakuwa *vichaka vya waharifu* na kupelekea huvunjivu wa amani na kuleta hofu kwa wakazi. Walinzi wa maeneo haya hawana muda wa kujadili na kujua kosa limetendwa kwa bahati mbaya au

makusudu, umetenda kosa au la hasha! Utajikuta upo kituo kikubwa cha polisi. Hawana simile kama wafanyavyo walinda usalama katika maeneo ya '**low density'**. Hivyo kuwa sawa na nyoka wakali wa porini lakini hufanya hivyo mara nyingine ni kwa ajili ya *kujihami*.

Pia maeneo yenye '**squtters**' hakuna usalama kabisa! Hata mharifu ukimuona au kumdhuru mtu, wakazi hushindwa kumkamata na kumtia hatiani kwa kuwa hakuna njia ya kupita na kumfuata mharifu huyo ili akamatwe. Pia kiusalama ni heri kusamehe kuliko kufuatilia sababu unaweza kudhurika zaidi kuliko hasara iliyotokea kama vile kichakani. **Vichaka** vyenyewe vinauwezo wa kutishia usalama na endapo kiumbe chochote kitapita kinaweza kujeruhiwa kwa kuchomwa na miiba kali za miti hiyo.

### 2.1.3 MAZINGIRA

Maeneo ya misitu ni masafi na tulivu, unyevu (mvua, mito, chemchem na vivuli) hufanya eneo kuwa la kijana na kuvutia. Hakuna kelele zaidi ya sauti nzuri za ndege na makundi ya nyuki na majani. Mpita njia, humpa mshangao 'mesmerized', na tabasamu la woga, muda mwingi hupata misisimko ya hofu. Alikadhalika katika makazi ya kitajiri (**low density**); makazi yanakuwa safi na tulivu ingawa wakazi ni watumiaji wakubwa wa bidhaa za viwandani. Ardhi yake hufunikwa na uoto wa kijana. Kwa kuwa wakazi wake wana uwezo / kipato mkubwa kumudu kuweka mazingira safi. Pia utulivu ni mkubwa katika makazi haya, sauti za ndege wanaofungwa na waasili pekee ndiyo husikika na kuonekane hivyo kuendelea kupamba eneo hilo mfano ndege Tausi na Kasuku katika mtaa wa Posta na Samora jijini Dar es salaam. Ingawa mazingira haya safi yanaweza kuharibiwa endapo;

**Misitu**: Uchomaji moto misitu na kupelekea kuota nyasi (plant seccession) na kwenye *makazi ya binadamu*, endapo sheria italegezwa na kuruhusu wakazi kutumia ardhi wapendavyo. Mfano baada ya kujengwa nyumba moja katika kiwanja kimoja, mmiliki anaanza kukata eneo lake na kuliuza na mwishowe mtaa unaanza kujaa wakazi na madhari hubadilika kama ilivyosasa kwa mitaa mingi ya miji na majiji ya Tanzania.

**Mapori (**mbuga**):** Uoto wake ni mchanganiko yaani miti, nyasi majani na fungus kama uyoga vinapatikana huko. Hakuna madhari ya kuvutia, ukame hasa kipindi cha kiangazi hubadili muonekano na miti kukauka kisha kuwa kama jangwa. Hivyo viumbe wa eneo hili hupata shida na wengine kuhama na kwenda maeneo mengine kutafuta maji na malisho. Maeneo ya '**high density'** mazingira hukosa mvuto kwa kuwa na mirundikano ya takataka, wingi wa watu, kelele na vurugu. Watu wenye kupenda utulivu na wenye magonjwa yanayohitaji utulivu mfano 'Blood pressure' wanahama na kwenda kutafuta utulivu sehemu nyingine hasa nje ya mji.

Hali hii ya kufanana kwa makazi ya miti na mtu ni dhahiri kwamba mipango miji ya makazi ya binadamu imeigwa toka kwenye makazi ya miti. Kwa sababu miti haiwezi kujifunza kitu chochote kutoka kwa mtu.

## 2. 2.0 NADHARIA YA MAISHA “UHAI”

KUZALIWA HADI KUFA

**USHAHIDI WA MLINGANO WA MAISHA YA MTI NA MTU**

### 2.2.1 MBEGU

Miti inatokana na mbegu na binadamu wanatokana na mbegu. Kurutubishwa kwa mbegu hizo kunategemea kiumbe cha kiume “male” kwenda kwa kiumbe cha kike “female”.

### 2.2.2 UKUAJI

Ustawi wa miti unahitaji vitu kama ardhi yenye virutubisho (rutuba) na tambalale, mwanga kwa ajili ya mmea huo kujitengenezea chakula (Photosynthesis), hewa (Carbondioxide), unyevu (maji). Matunda yanapatikana baada ya viumbe hawa kukomaa.

*Wakati kwa binadamu* ***(mtu);*** Ili kukua vizuri anahitaji chakula bora 'balance diet', hewa safi (Oxygen), mwanga wa jua/ nguvu za jua, na kupata matunda (watoto) baada ya kukomaa.

*Uwezo*; Elimu ndiyo itakayompa uwezo binadamu kumudu kujitafutia chakula na kutawala dunia. Kiwango cha uwezo wake ndiyo utakaoonesha ukubwa wa utawala wa dunia na binadamu wenzake. Alikadhalika kwa miti hutegemea kiwango cha mwanga wa jua katika kujitengenezea chakula (photosynthesis), miti inayopata mwanga ndiyo yenye nguvu ya kutawala ardhi. Kwa mfano kwenye misitu miti yenye nguvu ya kupata mwanga ndiyo inayotawala eneo.

**MATOKEO/ USHAHIDI**

*Matunda* hutoa sharubati ambayo ni lishe bora, ni malighafi (dawa), bidhaa, matibabu, chakula kwa viumbe wengine (wadudu, ndege, wanyama, mtu). Hivyo kuendesha maisha ya viumbe hivyo. Sawa na na watoto wa Mtu hupata wasomi/wataalamu mbalimbali na kusaidia kuendesha maisha ya viumbe vyote duniani.

### 2. 2.3 UVUMILIVU WA MAZINGIRA

Mfano mkubwa ni mti wa mkoko hauwezi kuishi na kukua vizuri nje ya pwani. Hata misitu ya kawaida inamea vizuri kutegemeana na hali ya hewa rafiki kwa msitu huo. Kuna msitu unaostahimili hali ya joto na mvua nyingi mfano misitu ya Kongo na misitu inayopatikana maeneo ya Afrika mashariki. Ukanda wa baridi una misitu inayovumilia hali hiyo.

**Ushahidi;**

Watu wanaoishi ukanda wa Kiikweta na Kitropiko wamezoea joto hivyo ni vigumu kuishi kwenye ukanda wenye baridi kali na kinyume chake.

Miti inapukutisha majani yake kipindi cha ukame ili kuhifadhi maji na chakula. Kama binadamu anavyohifadhi vyakula ghalani na maji kwenye matenki ili vitumike msimu wa ukame ambao sio rafiki kwa uzalishaji.

## 2.3 ASILI/ KURITHI

Mtu anapozaliwa kwenye familia duni, atasoma shule za hali duni, ataishi maisha duni, atakosa mahitaji muhimu lakini utavumilia na kusonga mbele. Hata akifanya vizuri bado atapata shida katika kupata kazi na akipata kazi, ni vigumu kupanda cheo cha juu (kuongoza) na ikitokea amepata uongozi; changamoto ni nyingi kwa sababu zilizobainishwa kwenye Kielelezo: Jendwali 1.1

## MATOKEO/ USHAHIDI

Miti yenye kutoa mbao ngumu, magome yenye kutengenezewa tiba, matunda matamu, na chakula ndiyo inayoshambuliwa. Endapo yatakosa ulinzi, inaweza kutoweka na miti yenye matunda matamu inaweza kushindwa kuendelea kutoa matunda hayo. Hali hiyo ni sawa na mtu aliyezaliwa kwenye familia duni na kukosa wasaidizi wakutengeneza mazingira mazuri ya elimu au kazi /mtandao.

Miti ya asili inaangamizwa hata kama ina umuhimu mkubwa katika viumbe vilivyokaribu na maeneo hayo kama kuwa hifadhi ya vyanzo vya maji na umuhimu wa mti kutokana na ubora wa mazao yake mfano mti wa mninga, mbambakofi, mivule na mikoko. Misitu ya kupandwa inakuwa haishambuliwi ingawa kuna uwezekano wa miti hiyo isiwe na sifa wala huhitaji mkubwa kwenye kupata mazao. Kama ilivyo rahisi kwa mtu anayetoka kwenye asili ya familia duni kunyimwa haki ingawa sifa na vigezo vinavyostahili kisheria anaweza kuwa navyo. Hivyo anaendelea kuwa msonobari bora (maskini mwerevu) katika mvule au mtomondo (matajiri/ mamlaka). Haiwezekani kuzaliwa msonobari na kufa mtomondo.

Mti unaweza kupotea na kumea kwenye msitu wa aina nyingine ya miti au hali ya hewa. Mfano; mtomondo kuota jangwani kisha kumudu kustahimili mazingira.

Mtu anaweza kulea mtoto anayetokana na asili nyingine na kukua ingawa hatopoteza asili yake.

**Ushahidi:** Miti iliyobebeshwa inazaa/kutoa matunda ya mti wa asili na endapo mti mpya una asili inayofanana na ya mwanzo matunda yake yatakuwa ni chotara na sio asili moja. Sawasawa na mtu, akilea mtoto asiye mzaa kwa mazingira mazuri au mabaya, mtoto atakua lakini hatopoteza asili yake ingawa inaweza kudumazwa au kuboreshwa kutegemeana na malezi aliyokulia. Mfano asili ya

uchapakazi, akili nyingi, kipaji, magonjwa ya kurithi, uvivu, rangi, asili ya utajiri au maskini. Mwenye asili ya umaskini, hata akipewa mali anaweza kutapanya na kufilisika. Alikadhalika mtoto mwenye asili ya kitajiri aliyelelewa kwenye familia ya kimaskini anaweza kutajirika hata kama hatoweza kufikia kiwango alichostahili. Asili ya kipato imejificha kutokana na mwingiliano wa watu; uhusiano wa mapenzi hauchagui asili bali malezi ndiyo yanayozingatia asili.

## 2.4 MAJANGA NA ASILI

(NADHARIA YA MABADILIKO YA MWENENDO WA MAISHA**)**

Moto, mafuriko, tetemeko, ukame, kimbunga, Tsunami:

Misitu huteketea na kuangamia na majanga haya sawa na mtu. Pia mtu anapoanzisha janga jingine 'vita' na kuangamiza maisha ya watu na mali zao.

Vita kwa watu na moto kwa misitu huleta matokeo yaliyosawa. Baada ya vita mfumo wa maisha ya mtu yanabadilika. Alikadhalika kwa miti (msitu) unapoungua moto, kuna mabadiliko makubwa na mara nyingine ni ngumu kutengeneza msitu mpya na kubakia mapori yenye mchanyaniko wa nyasi na miti mbalimbali.

Kama hatua madhubuti hazitachukuliwa za kukomesha (kuvumiliana kati ya matabaka yanayogombana) vita kwa mtu na moto kwa misitu (sheria) kuna kuwa na tabia ya kujirudia rudia (endless). Hivyo baadhi ya vizazi vya asili kupotea na eneo kutawaliwa na wageni na tabia za kigeni au mifumo ya maisha ya kigeni kuanzishwa.

**Ushahidi**: Nyasi haziwezi kumea msituni hadi itokee hali itakayosababisha miti kusumbuliwa na kupungua "Plant succession

## 2.5 MATUNZO/ULINZI

Adui mkubwa wa miti ni Mtu wakati Mtu anahitaji matunzo na ulinzi kusimamia malezi na usalama wake. Hivyo kuwepo kwa misitu ya hifadhi, mapori ya akiba, sheria ya vyanzo vya mito kutawezesha kuwa na dunia halisi yenye miti ya matunda matamu na salama, mbao ngumu, dawa zenye uwezo wakutibu pamoja kusafisha hewa na kufanya dunia kuwa pahala pazuri pa kuishi kwa viumbe vyote hai. Wakati huwepo wa vyombo kama vile shule, mahakama, hospitali, miundombinu, kanisa, na misikiti, malezi katika maadili mema ndiyo ulinzi imara kwa mtu.

Unataka mwanao awe mti gani? Upo uwezekano wakuzaa mtiki na malezi yakambadilisha kijana na kuwa na tabia za mbuyu ambao ni mti mkubwa sehemu kame na hauwezi kupata kuni achalia mbali mbao na mazao mengine ya miti. “*Ukiyaona maji na una kiu, lazima utayanywa.”*

.

Mabadiliko hayo toka mtiki hadi mbuyu ambao ngano za Kiafrika zinasema “kila shetani na mbuyu wake” kwa maendeleo huwezi kuchagua mbuyu ili kupata mabuyu pekee. Mabuyu ni kuwa na mtoto kwa matokeo ya idadi lakini watoto hao au huyo anakuwa hana mafanikio toka kwake. Wanazuoni waliotangulia wamefafanua vizuri kuhusu makuzi ya watoto na uwezo wao wakufikiri na matendo wayapendayo kwa kila umri pamoja na madhara ya matendo hayo (Jean Piaget).

**USHAHIDI**

Mtoto wa mhandisi hawezi kuwa mhandisi kwa sababu mtoto wake hakulelewa kama alivyolelewa yeye na wazazi wake.

Mzazi tajiri akifariki na mali zake huanza kupotea sababu warithi wake hujengwa *kutumia na sio kuzalisha.*

Misemo ya Kiswahili “Samaki mkunje angali mbichi” na “mfundishe mtu kuwinda na sio kula nyama”

**MASWALI**

Hadi mtoto anatoroka na kuingia mtaani, mzazi/mlezi anakuwa yuko wapi?

1. Je, huo ndiyo ulinzi kamili wa misitu yetu?
2. Je, sheria za nchi na dunia pekee zitaweza kulinda hadi kwenye kuta za nyumba yako?
3. Je, msitu utapatikana?

Umri wa utu umzima:

1. *Nani atayekubali mabadiliko yake*?
2. Kitu gani kitawaaminisha watu kuwa anaweza kuongoza ikiwa yeye alishindwa kufuata sheria na taratibu za shule au familia, vipi ataweza kuzingatia sheria za nchi au kimataifa?
3. Wale alioshirikiana nao katika maovu atawachukulia vipi?

**USHAHIDI**

- Baadhi ya wazazi wa viongozi kutoishi, kutembelea wala kushereheka na watoto wao.
- Mazishi ya kuchelewa ili kufanya maandalizi ya kuandaa mazishi.
- Mshtuko mdogo kwa wanakijiji husika; wanakijiji kuendelea na shughuli zao za kila siku endapo unatokea msiba wa kiongozi wakati wanajamii husika walitakiwa kuwa na huzuni kwa kwa kuwa aliyefariki ni ndugu yao.
- Wengine huwakana ndugu na jamaa zao. Pia kutokutembelea vijijini kwao kwa sababu wanayafahamu yale yote waliyoyatenda kabla ya nafasi hiyo. Aibu, wasiwasi, hofu na kutojiamini.
- Kushiriki kuwachafua viongozi au watendaji walio wema.
- Viongozi kujenga makazi/Ikulu zao binafsi mijini au nje mbali na kwao
- Viongozi wa Kiafrika utambulisho wa watoto unabaki kuwa wa watoto wachache wakati wanao wengi.

**MATUNDA BORA**

Elimu (maisha): utambuzi wa mambo/ajira

Teknolojia: mashine, vifaa, mitambo/ viwanda, mawasiliano kama simu, media, (mitandao ya kijamii) Uongozi bora

Kutengeneza mifumo ya uendeshaji / huduma za kijamii na maendeleo: elimu, afya, uongozi, uchumi; benki, taasisi, mazingira.

*Matunda haya hunufaisha dunia mzima kama ilivyo hasara kwa dunia.*

MFANO; Kuna aliyegundua ujenzi wa nyumba bora, leo kila Mtu huishi kwenye nyumba bila kujali ubora wa nyumba hiyo.

**Ushahidi:** Viongozi wakuu wa nchi kama vile Rais, mzazi anapoteza mamlaka ya uzazi na kuliacha jukumu hilo kuwa la nchi mzima.

## 2. 6 TABIA KATI YA MITI NA MTU

*Vichaka*: matendo kiharifu

*Mwarobaini*: mtoto/ mtu / watu wenye manufaa, tiba, watatuzi wa migogoro, wasuruhishi, wakombozi, watetezi

Matunda mema yanatengenezwa: Jamii iliyoelimika

Miti iliyostawi vizuri ina vutia amani: Ishara ya amani miongoni mwa watu wakati miti angavu na isiyostawi ina karibisha wanyama wakali, na wadudu. Sawa na mtu, maisha kwenye familia zenye uwezo mshikamano na migogoro haiko wazi. Lakini familia maskini ukaribisha utengano na migogoro iliyo wazi.

Kiini kikubwa: mfano mpingo ni uimara. Wakati kwa mtu ni busara na hekima

Magamba (magome): ulinzi, kiafya, kimatendo mabaya au mema

Kupukutisha majani: kuhifadhi fedha uchumi wa taifa au mtu binafsi kama mti sababu unapokuwa na ziada unahifadhi kingine kwa kupunguza matumizi.

## JENDWALI 1.1 MFANANO WA ASILI YA MITI NA MTU

| **HALI YA MAJI** | **UKAME (DRY)** | **UNYEVU (WET)** | **MAJI BARIDI / CHUMVI (ardhi chepechepe)** |
|---|---|---|---|
| Aina ya miti | ○ Mbuyu<br>○ Msonobari<br>○ Mwanzi<br>○ Mpingo<br>○ Sega<br>○ Cactus<br>○ Mbigili | ○ Mvule<br>○ Mbambakofi<br>○ Mkwaju<br>○ Mtiki<br>○ Mkwinini | ○ Mtomondo<br>○ Mkoko na Mkandaa (maji chumvi) |
| **Daraja la kipato (Mtu) Mfano wa shughuli zao**<br>Asili ya makazi | **Kipato cha kujikimu (Squatters)** | **Maisha ya kipato cha kati (High density)** | **Kimamlaka au kipato cha juu (Low density)** |
| | ○ Ukulima mdogo<br>○ Ufugaji mdogo<br>○ Uvuvi mdogo<br>○ Ujasiriamali<br>○ Wafanyakazi wa ngazi ya chini na kawaida<br>○ Wasiofanyakazi | ○ Waajiriwa<br>○ Watumishi wa serikali wa ngazi ya kati mfano; kuanzia wakuu wa Idara<br>○ Maafisa katika taasisi, mashirika ya umma au binafsi<br>○ Viongozi katika ngazi za serikali<br>○ Talanta<br>○ Wataalamu | ○ Viongozi wa ngazi za juu<br>○ Wafanyabiashara wakubwa<br>○ Familia za kifalme<br>○ Talanta<br>○ Wenye akili nyingi |

***

# REJEA


Abercrombie P. (1910), MODERN TOWN PLANNING IN ENGLAND: A COMPARATIVE REVIEW OF "GARDEN CITY" SCHEMES IN ENGLAND, Liverpool University Press. Https://www.jstor.org/stable/40100517

Abercrombie P. and Reilly C. R, (1910), TOWN PLANNING SCHEMES IN AMERICA, Liverpool University Press
Https://www.jstor.org/stable/40100521

Adshead S. D, (1910), AN INTRODUCTION TO CIVIC DESIGN, Liverpool University Press. Https://www.jstor.org/stable/40100516

Charles Barnes and Martin Kamen, (2002), PHOTOSYNTHESIS RESEARCH, Kluwer Academic Publishers 73:7-10, 2002

Hans Lambers, PLANT REPRODUCTIVE SYSTEM, University of Western Australia, Crawley, Western Australia.

Henggeler, Scott W. et all, (1998), MULTI-SYSTEMIC TREATMENT OF ANTI-SOCIAL BEHAVIOR IN CHILDREN AND ADOLESCENTS, New York – USA

Https://www.doi.org/10.1007/978-3-030-45381-7_6

John C. Maxwell, THE 21 IRREFUTABLE: LAWS OF LEADERSHIP Limited Edition, Manu Graphics Books, New Delhi, India.

Marquis F. J, (1910), TOWN PLANNING SCHEMES IN AMERICA, Liverpool University Press
Https://www.jstor.org/stable/40100523

Oxford, (2015), ADVANCED LEARNER'S DICTIONARY, New 9th Edition, Oxford University Press, United Kingdom.

Pavel N. Davidenko and Davies H.W, (1990), THE EFFECTIVENESS OF SETTLEMENT PLANNING: TOWN PLANNING NORMS AND STANDARDS IN THE CMEA COUNTRIES, Liverpool University Press

TECDEN, (2013), KIUNZI CHA MALEZI MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA MTOTO, Tanzania ECD Network, Dar es Salaam – Tanzania Https://www.ecdnetwork.org

Willy Digital Archives, (2016), PHOTOSYTHESIS: NEW APPROACHES TO THE MOLECULAR, CELLULAR, AND ORGANISMAL LEVELS, The New York Academy of Sciences. ISBN: 9781119084150

Yanghee Lee, (2009), "MWONGOZO WA MALEZI MBADALA YA WATOTO", Umoja wa Mataifa, Seoul, Korea

**TOVUTI**


Https://www.britannica.com
Https://www.ncert.nic.in/textbook/gescl12.pdf Reproduction in plants

Http://www.iium.edu.myzhadithzooqmt 17/11/2005

Http://www.estrellamountain.edu.photosynthesis 30/1/1998

Https://www.vetmed.tamu.edu/macawproject/volunteer/health-and-safety-in-the-jungle

Https://www.zmescience.com

Https://www.eartheclipse.com Types of forests

Https://www.onetreeplanted.org/blogs/stories/types-of-forests

Https://www.jstor.org/stable/40112950

Https://www.settlementplanners.com

Https://www.unhcr.org

Https://www.4structures.com

Https://www.amicusplanners.com

Https://www.tcmtreatment.com

Https://www.breathing.tips/experrrrrience/breathing

Https://www.Mitiki.blogspot.com/2009/06/atupa-dawa-ya-kuulia-wadudu.html 7 Juni, 2009

Https://www.imtmherbal.blogspot.com 10 Juni, 2016

Https://www.tibaherbs.wordpress.com 12 Mei, 2013

Https://www.bufadeso.blogspot.com 2 Desemba, 2015

Https://www.tanzaniagateway.org

Https://www.jamii.go.tz

Https://www.wvi.org/tanzania Ulinzi wa mtoto Booklet

Https://www.esrf.or.tz

Https://www.tie.go.tz 2009

Https://www.youthpolicy.org Desemba, 2007

Https://www.sos-childrensvillagestanzania.org